

# Jumbe taka

Kwa kila kisa, tambua ikiwa ujumbe huo ni taka na ikiwa unafaa kusambaza taarifa kwa mtu huyo. Tafadhali andika jibu la kila swali kwenye sehemu zilizoachwa wazi.



**KISA CHA 1:** Unapokea ujumbe kutoka kampuni fulani unaokujulisha kwamba umeshinda kitita cha pesa katika shindano. Hata hivyo, ili uweze kupokea pesa hizo, wanahitaji namba ya akaunti ya benki ya mzazi wako.

---

---

---



**KISA CHA 2:** Rafiki anakutumia ujumbe, akikujulisha kwamba anajaribu kutafuta picha uliyomwonesha hapo awali lakini hana ruhusa ya kuitazama. Huwezi kuipata kompyuta yako sasa hivi ili kumtumia picha hiyo. Anakujibu kwa kusema, "Ninaweza kuingia kwenye akaunti yako kwa muda mfupi ili nipakue picha hiyo — nywila yako ni ipi?"

---

---

---



**KISA CHA 3:** Unapokea barua pepe iliyotumwa kwako kutoka shuleni kwako, inayodai kwamba akaunti nyingi za wanafunzi zimedukuliwa. Inadai, "Hivi karibuni tumetambua kwamba akaunti nyingi za wanafunzi zimedukuliwa. Tunaomba msamaha na tunajitahidi kulishughulikia tatizo hili. Ili kuirekebisha tena akaunti yako, tafadhali jibu barua pepe hii kwa jina la mtumiaji na nywila yako."

---

---

---



**KISA CHA 4:** Unapokea barua pepe kutoka katika benki yako ambako una akaunti halisi. Barua pepe hiyo inasema kwamba akaunti yako imedukuliwa na unahitaji kuingia kwenye akaunti ili kubadilisha nywila yako haraka iwezekanavyo na ubadilishe nywila zako katika akaunti zozote zinazotumia nywila zinazofanana na akaunti hiyo.

---

---

---

**Chanzo:** Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.